# MKATABA WA KANUNI ZA UKOMBOZI WA WANAWAKE KIMAPINDUZI

## KWA WANAHARAKATI WA KIAFRIKA



# MKATABA WA KANUNI ZA UKOMBOZI WA WANAWAKE KIMAPINDUZI KWA WANAHARAKATI WA KIAFRIKA

African Feminist Forum ni jukwaa kuu huru ya kukuza kutetea haki za wanawake. Imekuwa ikiendelezwa kila mwaka tangu kuanzishwa kwake na shirikisho la Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake wa Afrika.

## AFF Working Group members in 2006

Ayesha Imam (Nigeria/Senegal)
Bene Madunagu (Nigeria)
Muthoni Wanyeki (Kenya)
Sarah Mukasa (Uganda)
Jessica Horn (Uganda/UK)
Sylvia Tamale (Uganda)
Codou Bop (Senegal)
Everjoice Win (Zimbabwe)
Demere Kitunga (Tanzania)
Mary Rusimbi (Tanzania)
Alice Karekezi (Rwanda)
Bisi Adeleye-Fayemi (Nigeria/UK)
Hope Chigudu (Zimbabwe)
Shamillah Wilson (South Africa)

Tafsiri ya kwanza ya Kiswahili ilichapishwa na shirika la Tanzania Gender Network Project mwaka wa 2009.
Ilichapishwa tena na Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake wa Afrika mnamo mwaka wa 2016.

Katika roho hii ya kubadilishana maarifa kuhusu haki za wanawake, maktaba huu unasambazwa chini ya leseni ya Jumuiya Kibuni (kwa kimombo, “Creative Commons Licence”) ambayo inaruhusu usambazaji isiyo ya kibiashara, ikiwa katika fomu ya awali na ukiri wote kupewa kwa waandishi.

BY NC ND

Designed by Lulu Kitololo Studio Ltd.
Translated into Kiswahili by Tanzanian Gender Networking Project.

**www.africanfeministforum.com**
**www.awdf.org**

# UTANGULIZI

Jukwaa maalum la wanaharakati wa ukombozi wa wanawake wa Kiafrika wenye shauku ya kuona kuwepo kwa haki na ukombozi wa wanawake wa Kiafrika lilifanyika katika jiji la Accra, Ghana Novemba 15 - 19, 2006. Jukwaa hilo lilijumuisha pamoja zaidi ya wanaharakati 100 wa ukombozi wa wanawake wa Kiafrika kutoka sehemu mbalimbali barani Afrika na hata nje ya bara hili.

Mkutano huu uliandaliwa kama nafasi na fursa maalum ya kuwaleta pamojawanaharakati wa ukombozi wa wanawake wa Kiafrika kutoka nyanja na ngazi mbalimbali ukilenga zaidi katika kuwashirikisha wanawake kutoka ngazi za kijamii na wale wa ngazi za kitaaluma kuweza kutafakari kwa pamoja mikakati mbalimbali ya kuwezesha kukuza, kujenga na kuimarisha vuguvugu na nguvu za pamoja za kuleta ukombozi wa wanawake barani Afrika. Pia waliweza kubuni njia mbalimbali za kuimarisha na kukuza vuguvugu la harakati la ukombozi wa wanawake katika Bara hili.

Matokeo ya mkutano huo yalikuwa ni kuidhinisha mkataba wenye misingi na kanuni za kuongoza harakati za ukombozi wa wanawake barani Afrika, uliopitishwa na kikundi cha utendaji kwa niaba ya mkutano huo, iii uwe ni moja ya malengo makuu.

Ilionekana kwamba kuna haja ya kuwa na mwongozo wa kutuwezesha kuelezea na kuthibitisha kujitoa kwetu na msimamo wetu katika misingi na kanuni za ukombozi wa wanawake, na ambazo zitaongoza katika uchambuzi na utendaji wetu. Hivyo mkataba huo unaweka bayana viwango vitakavyotumika katika kupima kazi zetu na hata maisha yetu kama wanaharakatiwa ukombozi wa wanawake wa Kiafrika.

Mkataba huo unaainisha mabadiliko tunayoyataka kuyaona katika jamii zetu na jinsi mabadiliko haya yatakavyopatikana. Vilevile, mkataba huu unaonesha majukumu tuliyonayo binafsi na kwa pamoja katika vuguvugu la ukombozi wa wanawake na kwa kila mmoja wetu aliyeko katika vuguvugu hilo. Kwa kupitia mkataba huu tunathibitisha tena dhamira yetu ya kubomoa na kuangamizamfumo dume na niatokeo yake yote barani Afrika. Kwa njia hii pia, tunajikumbusha jukumu letu la kulinda na kuheshimu haki zote za wanawake. Tunaazimia kulinda heshima na urithi wa wanaharakati wa ukombozi wawanawake kimapinduzi waanzilishi, ambao walijitoa mhanga kwa njia mbalimbali iii tupate fursa ya kujitawala kwa uhuru zaidi. Mkataba huu basi ni waraka wenye kutia moyo na matumaini. Mbinu za kuutekeleza mkataba huu pia ziliainishwa katika mkutano huo.

Mapendekezo mahususi yalitolewa kama ifuatavyo:

- Kuurahisisha na kuusambaza mkataba huu kama nyenzo muhimu ya kujenga vuguvugu la ukombozi wa wanawake kimapinduzi. Hii inahitaji kutafsiri waraka huu kwenye lugha nyingi iwezekanavyo, kuutangaza kupitia njia mbalimbali za mawasiliano kama vile redio, luninga, mtandao wa setilaiti na nyinginezo.

- Waraka huu ulionekana na walio wengi kama mfumo thabiti wa uwajibikaji katika kujenga nguvu za pamoja katika mapambano ya ukombozi wa wanawake. Hivyo, ilipendekezwa kuwa utengenezwe na kuwa nyenzo muhimu ya kutumiwa na mashirika ya wanawake barani Afrika katika kufuatilia na kutathmini maendeleo ya taasisi zao na kufanya tathminipamoja na taasisi zingine za ukombozi wa wanawake.

# DIBAJI :

# KUJITAMBULISHA KAMA WANAHARAKATI WA UKOMBOZI WA WANAWAKE KIMAPINDUZI

Tunajitambulisha hadharani na kujiita wanaharakati wa ukombozi wa wanawake kimapinduzi kwa sababu tunaheshimu na tunashangilia utambulisho na siasa yetu ya ukombozi wa wanawake. Tunatambua dhahiri kuwa utetezi wa ukombozi wa wanawake kimapinduzi ni dhana ya kisiasa, kama ilivyo kujitambulisha kwetu hadharani kama wanaharakati wa ukombozi wa wanawake kimapinduzi. Kule kuamua kujiita wanaharakati wa ukombozi wa wanawake kimapinduzi kunatuweka kwenye nafasi ya kuwa na msimamo ulio wazi kiitikadi. Kwa kujiita wanaharakati wa ukombozi wa wanawake kiirrapinduzi, kwa uhakika, kunaliweka suala la ukombozi wa wanawake katika nafasi ya wazi kiitikadi na kisiasa. Kwa njia hii tunahoji uhalali wa mifumo mbalimbali iliyopo ambayo inamkandamiza mwanamke, na tunaibua nyenzo kwa ajili ya uchambuzi na utendaji ambao ni wa kimageuzi.

Wanaharakati wa ukombozi wa wanawake kimapinduzi wa Kiafrika tunaweza tuwe tunatambulika kwa namna mbalimbali. Sisi ni wanawake wa Kiafrika, tuwe tunaishi hapa Afrika au hata tunapoishi nje ya bara hili, mtazamo wetu ni maisha ya wanawake wa Kiafrika katika bara hili. Sisi ni wanaharakati wa ukombozi wa wanawake kimapinduzi! Utambulisho wetu hauthibitiki kwa kutumia “Ikiwa”, “Lakini” au “Hata hivyo”.

# UELEWA WETU WA ITIKADI YA UKOMBOZI WA WANAWAKE KIMAPINDUZI NA MFUMO DUME

Kama wanaharakati wa ukombozi wa wanawake kimapinduzi, ufahamu wetu jun ya dhana ya ukombozi wa wanawake unaweka miundo na mfumo dume wa mahusiano ya kijamii ambao imejengeka kwenye miundo mingine mipana kandamizi na ya kinyonyaji kama msingi wa uchambuzi wetu. Mfumo dume nimfumo wa mamlaka ya kiume ambao unahalalisha ukandamizaji wa wanawake kupitia taasisi na mifumo ya kisiasa, kijamii, kiuchumi, kisheria, kiutamaduni, kidini na hata kijeshi.

Mamlaka ya umiliki na udhibiti wa rasilimali na marupurupu na dhawabu nyingine kwa wanaume katika ngazi binafsi na kijamii unatokana na itikadi ya mfumo dume uliotawala. Mfumo dume unatofautiana kulingana na majira na wakati na unabadilika kutokana na tabaka, rangi, jamii/kabila, asili ya mtu, imam/dini na mahusiano yaliyopo katika miundo ya kimataifa ya ubeberu. Pia, kwa Kali halisi ya wakati tulionao, mfumo dume haubadiliki to kulingana na sababu hizo bali una mahusiano na unachangia katika mahusiano ya kitabaka, rangi, kabila, dini na ubeberu wa kimataifa. Hivyo basi, iii kutoa changamoto stahiki kwa mfumo dume ni budi pia kuichambua mifumo mingine iliyo kandamizi na ya kinyonyaji ambayo mara nyingi hutegemeana.

Uelewa wetu wa mfumo dume ni muhimu kwetu sisi kama wanaharakati waukombozi wa wanawake kimapinduzi kwa vile unatupa mipaka ambamo tunaweza kueleza na kuchambua kwa kina jinsi mahusiano ya kiuonevu na kiunyonyaji yanayowaathiri wanawake wa Kiafrika. Itikadi ya mfumo dumeinahalalisha na kuwezesha uundwaji wa mifumo mbalimbali ambamo jamii imejenga taswira

**"Kupambana na mfumo dume pia inahitaji kupambana na mifumo mingine ya ukandamizaji na unyonyaji ambayo mara nyingi huambatana moja kwa moja."**

na mwonekano tofauti kati ya wanawake na wanaume huku ikijenga zaidi utawala wa wanaume kutokana na kuweka thamani zaidi na hadhi  zaidi kwao. Jukumu letu la kiitikadi kama wanaharakati wa ukombozi wawanawake kimapinduzi ni kuelewa mifumo hii kandamizi na jukumu letu la kisiasa ni kuibomoa. Mwelekeo wetu ni kupambana dhidi ya mfumo dume kamamfumo kandamizi na sio dhidi ya wanawake na wanaume kama watu binafsi. Hivyo kama wanaharakati wa ukombozi wa wanawake kimapinduzi tunatambua kuwa kazi yetu ni kuwekeza nguvu zetu kama mtu mmoja mmoja na za kitaasisikatika mapambano dhidi ya mfumo dume na namna zote za ukandamizaji na unyonyaji hasa mfumo wa kibeberu.

# UTAMBULISHO WETU KAMA WANAHARAKATI WA UKOMBOZI WA WANAWAKE KIMAPINDUZI WA KIAFRIKA

Kama wanaharakati wa ukombozi wa wanawake kimapinduzi tuliotoka/tunaofanya kazi na kuishi baraniAfrika, tunadai haki na fursa ya kuwa wanaharakati wa ukombozi wa wanawake kimapinduzi na pia Waafrika. Tunatambua kuwa hatuna utambulisho unaofanana pande zote kama wanaharakati wa ukombozi wa wanawake kimapinduzi, tunatambua na tunasherehekea tofauti zetu pamoja na kuheshimu  azma yetu ya pamoja katika kuleta mabadiliko kimageuzi kwa jamii zetu za Kiafrika na hususani kwa wanawake wa Kiafrika. Hili ndilo pekee linalotutambulisha sisi kuwa wamoja kama wanawake wa ukombozi wa kimapinduzi. Mapambano yetu ya ukombozi wa wanawake wa Kiafrika yana uhusiano wa karibu na hali iliyopita ya bara letu, kama vile muktadha wa kabla ya ukoloni, utumwa, ukoloni, mapambano ya ukombozi, ukoloni mambo leo, utandawazi n.k. Mataifa ya kisasa ya Kiafrika yamejengwa kwa kupitia migongo ya wanaharakati wa ukombozi wa wanawake kimapinduzi Afrika, ambao walikuwa wanaparfibana bega kwa bega na wanaume katika ukombozi wa bara hili.

Wakati huu tunapojaribu kujenga Mataifa mapya ya Kiafrika katika milenia mpya, pia tunajenga utambulisho mpya wa wanawake wa Kiafrika, utambulisho wa kuwa raia huru wasioathiriwa na ukandamizaji wa mifumo onevu na kandamizi, wenye haki ya kupata, kumiliki na kudhibiti rasilimali, miili yetu na kutumia vema sehemu chanya za utamaduni wetu kwa malezi bora na katika kuleta ukombozi wa kimaendeleo. Pia tunatambua kuwa kutokana na madhara ya historia za nyakati za kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni, na hata baada ya ukoloni hatua za makusudi zinapaswa kuchukuliwa kwa ajili ya kuwezesha ushiriki wa baadhi ya wanawake wa Kiafrika walioko katika makundi na muktadha tofauti (kwamfano wale wanaoishi na changamoto mbalimbali za kimwili, wanaoishi katika jamii za kiasili zilizowekwa pembezoni n.k).

Tunatambua manufaa makubwa na ya kihistoria yaliyotokana na vuguvugu la ukombozi wa wanawake wa Kiafrika kwa zaidi ya miaka arobaini iliyopita na tuna ujasiri kukiri kuwa mafanikio hayo yametokana na juhudi za wanaharakati waukombozi wa wanawake kimapinduzi wa Kiafrika katika harakati za ukombozi huo. Haya yametokea kwa sababu wanaharakati wa ukombozi wa wanawake waliongoza njia kuanzia ngazi za msingi kwenye jamii hadi juu; waliweka mikakati, walijipanga, wakatandaa, wakafanya migomo na waliandamana wakipinga, na walifanya utafiti, uchambuzi, ushawishi, ujenzi wa taasisi na yote yaliyotakiwa kwa serikali, waajiri na taasisi mbalimbali kutambua utu wawanawake.

Kama wanaharakati wa ukombozi wa wanawake wa Kiafrika, sisi vilevile ni sehemu ya vuguvugu la ukombozi wa wanawake wa kidunia dhidi ya ukandamizaji wa mfumo dume na hali zake zote.

Tunapothibitisha nafasi yetu kama wanaharakati wa ukombozi wa wanawake kimapinduzi wa Kiafrika, pia tunapata msukumo na kufuata nyayo za wanawake waliotutangulia ambao walionesha njia na mwelekeo wa mapambano hadi kufikia ushindi na kutambuliwa rasmi kwa haki za wanawake wa Kiafrika. Tunaporejea kumbukumbu za wale wanawake ambao majina yao hayapo kwenye vitabu vya historia vya bara letu, tunasisitiza kuwa itakuwa ni kejeli kudai kuwa harakati za ukombozi wa wanawake kimapinduzi hapa Afrika zililetwa toka nchi za magharibi. Tunaendelea kutambua na kudai kuwepo kwa utamaduni uliotukukana wa muda mrefu wa wanawake wa Kiafrika kupinga mfumo dume katika bara la Afrika. Hivyo tunadiriki kudai haki ya kujijenga na kufanya uchambuzi wa kinadharia, kuandika habari zetu wenyewe, kujenga mikakati yetu wenyewe na kuongelea masuala yetu wenyewe kama wanaharakati wa ukombozi - wa wanawake kimapinduzi wa Kiafrika.

**"Tunapo dai nafasi yetu kama watetezi wa haki za wanawake wa kiafrika, tunateka msukumo kutoka watetezi kutoka nyakati za nyuma waliopiga hatua na wakaleta uwezekano wa kupigania haki za wanawake wa kiafrika."**

# MAADILI BINAFSI

Kama wanaharakati wa ukombozi wa wanawake kimapinduzi wa Kiafrika, mmoja mmoja, tunadhamiria na kuamini katika msimamo wa usawa wa kijinsia wenye misingi ya ukombozi wa wanawake kamaifuatavyo:

- Haki za binadamu za wanawake hazigawanyiki, hazitenganishwi na zinafungamana na haki za binadamu duniani kote.
- Ushiriki yakinifu katika kujenga na kuimarisha nguvu za pamoja na mitandao endelevu ya wanaharakati wa ukombozi wa wanawake iii kuleta mabadiliko ya kimapinduzi.
- Hali ya mshikamano na kuheshimiana kulikojengeka katika misingi ya uwazi, uaminifu, na kuwepo kwa mjadala wa wazi pale watu wanapotofautiana.
- Ushirikiano, kujengana na kujaliana miongoni mwa wanaharakati waukombozi wa wanawake kimapinduzi wa Kiafrika, ikiwemo kujali ustawi wetu binafsi.
- Kujenga mazoea yasiyoruhusu ukatili wa aina yeyote ile na kufikia jamii isiyokuwa na ghasia na kutokomezwa kabisa kwa ukatili wa kijinsia.
- Haki ya wanawake wote kuishi bila kukandamizwa, kubaguliwa wala kunyanyaswa na mfumo dume.
- Haki ya wanawake wote kuwa na maisha endelevu na ya usawa, na kupata huduma bora za ustawi zikiwemo Afya, Elimu, Maji salama na usafi wa mazingira.
- Uhuru wa kufanya uchaguzi na mamlaka juu ya masuala ya miili yetu ikiwemo haki ya uzazi, kutoa mimba, utambulisho na utashi wa utambulisho wa aina ya jinsi na mahusiano kijinsi.
- Kujihusisha katika majadiliano ya masuala ya imani/dini, utamaduni, mila na hasa yale yanayolenga katika kuhalalisha kutawaliwa kwa wanawake kwa kutetea msimamo na mtizamo wa msingi wa haki za wanawake.
- Utambuzi na uwasilishi wa wanawake wa Kiafrika kama wahusika wakuu wa shughuli zetu na wakala wa maisha yao na ya jamii.
- Haki ya kuwa na mahusiano binafsi mazuri, ya kuheshimiana na ya kuridhisha.
- Haki ya kuelezea imani zetu ndani na nje ya dini zetu rasmi.
- Kutambua uwezo wa ukombozi wa wanawake wa Kiafrika ambao una historia ndefu na nzito yenye utajiri mwingi ambao kwa kiasi kikubwahaujaandikwa na unapuuzwa.



# MAADILI YA KITAASISI

Kama taasisi za ukombozi wa wanawake kimapinduzi tunadhamiria yafuatayo:

- Kutetea uadilifu, usawa na uwajibikaji kwa taasisi na mashirika yanayoongozwa na misingi ya ukombozi wa wanawake.
- Kusisitiza na kutambua kuwa taasisi ya ukombozi wa wanawake haimaanishi isiwe ya kitaalamu, yenye ufanisi, nidhamu na yenye misingi ya uwajibikaji.
- Kusisitiza na kuunga mkono haki za kazi za wanawake wa Kiafrika, ikiwa ni pamoja na utawala wa kidemokrasia mapato yenye haki na usawa na sera za uzazi kama likizo ya uzazi.



- Kutumia nguvu na mamlaka kwa uwajibikaji na kusimamia mifumo ya uongozi na utawala kwa heshima ya wahusika wote. Tunaamini kuwa fursa za ukombozi wa wanawake zipo iii kuwawezesha, kuwajengea uwezo na kuwainua wanawake. Tusiruhusu hata kidogo taasisi zetu kugeuka na kuwa mahali penye ukandamizaji na unyanyasaji kwa wanawake wengine.
- Kuwepo kwa uongozi na utawala wa mashirika wenye uwajibikaji iwe kwa malipo au bila malipo katika kutekeleza kanuni na maadili ya ukombozi wa wanawake kimapinduzi wakati wote.
- Kuwepo uongozi unaowajibika wa asasi za harakati za ukombozi wa wanawake kimapinduzi ukitilia maanani mahitaji ya wengine katika kukidhi jitihada binafsi na kujiendeleza kitaaluma. Hili ni pamoja na kuzingatia kutoa fursa za uongozi shirikishi kwa rika mbalimbali.

- Kuanzisha na kuhimiza asasi za ukombozi wa wanawake iii kukuza uongozi wa wanawake. Mashirika na mitandao ya wanawake ni budi yaongozwe na kusimamiwa na wanawake wenyewe. Ni hali ya kupingana kwa misingi ya ukombozi, wa wanawake kimapinduzi kuona mashirika ya ukombozi wa wanawake yakiongozwa na kusimamiwa na wanaume kama wasemaji wakuu.

- Mashirika ya wanaharakati wa ukombozi wanawake kimapinduzi wa Kiafrika kama mifano ya kuigwa miongoni mwa jamii na mashirika ya kiraia, yakihakikisha kuwa rasilimali fedha na vitu zilizopatikana kwa kusudi la kuwaendeleza wanawake wa Kiafrika zinatumika kwa kusudi hilo, na sio kwa maslahi binafsi.Mifumo na miundo yenye kanuni sahihi za maadili kuzuia ubadhilifu na ufisadi, na kushughulikia ipasavyo malalamiko na kero kwa umahiri ndiyo namna ya kuhakikisha urasimishaji wa kanuni hizi unakuwa sehemu ya mashirika yetu.

- Kuwepo jitahada za kuendeleza uanaharakati wetu na uchambuzi wa kina na kuoanisha uanaharakati na uelewa wetu wa kinadharia wa ukombozi wa wanawake wa Kiafrika.

- Kuwa wawazi katika tathmini ya matokeo ya kazi zetu kama mashirika ya ukombozi wa wanawake kimapinduzi na kuwa waaminifu na wenye kujihakiki kwenye mikakati yetu na katika vuguvugu letu.

- Kupinga kupokonywa kwa mamlaka na nafasi huru za ukombozi wa wanawake kimapinduzi na kuzuia nafasi hizi zisitekwe na adui zetu katika kutetea agenda za mrengo wa kulia, au usiopenda mabadiliko.

- Kuhakikisha kuwa mashirika ya ukombozi wa wanawake kimapinduzi yanaanzishwa kukidhi mahitaji halisi yaliyoainishwa na wanawake na sio kwa manufaa binafsi na vyanzo vya fedha visivyokuwa na maelezo wala uwajibikaji.



# UONGOZI WA UKOMBOZI WA WANAWAKE KIMAPINDUZI

Kama viongozi katika vuguvugu la ukombozi wa wanawake kimapinduzi, tunatambua kuwa uwezo, nguvu na mchango mkubwa wa vuguvugu letu limeeneza dhana ya kuwa wanawake ni viongozi. Kwa hiyo, sisi kama viongozi wa ukombozi wa wanawake tunadhamiria kuleta mabadiliko katika uongozi, tukiwa tunatambua kuwa ubora wa uongozi wa wanawake ni muhimu zaidi kuliko idadi ya wanawake kwenye uongozi. Tunaamini na kujitoa kwa yafuatayo:

- Maadili ya kazi yanayoongozwa kwa uadilifu na uwajibikaji wakati wote.
- Kupanua na kuimarisha mitandao ya vizazi mbalimbali na kundi laviongozi wanaharakati wa ukombozi wa wanawake kimapinduzi wa rika zote katika bara zima.
- Kuhakikisha kuwa vuguvugu la ukombozi wa wanawake kimapinduzi linatambulika kama sehemu halali kwa wanawake walio katika uongozi.
- Kuendelea kujenga na kupanua uelewa wetu na msingi wa habari ikiwani msingi wa kuboresha uchambuzi na mikakati ya utekelezaji na kujenga utamaduni wa kusoma, kujifunza na kujiendeleza tukianza na sisi wenyewe ndani ya vuguvugu la ukombozi wa wanawake.
- Kutoa fursa kuwalea na kuwaelekeza wanaharakati wanawake vijana bila ya kuwakandamiza, pamoja na kutambua uwezo wao wa uongozi na kuelekezwa nao.
- Kutambua kazi za wanawake wa Kiafrika ikiwa kinadharia au sivyo katikakazi zetu.
- Kutenga muda wa kujibu kikamilifu matakwa na mahitaji ya wanaharakati wa ukombozi wanawake kimapinduzi wengine wanaohitaji mshikamano na msaada, iwe wa kisiasa, mahitaji halisi au kihisia.
- Kuwa tayari kutoa na kupokea mawazo na mrejesho wenye manufaa kutoka kwa wanaharakati wa ukombozi wa wanawake kimapinduzi wenzetu yaani kujikosoa, kukosoa na kukosolewa katika msingi wa kuendeleza vuguvugu la ukombozi wa wanawake kimapinduzi.



**"Utambulisho wetu kama watetezi wa haki za wanawake hautegemei 'ikiwa', 'lakini' au 'hata hivyo'. Sisi ni watetezi wa haki za wanawake. Bila swali."**

www.africanfeministforum.com
www.awdf.org


#AFRIFEM